RIHLATUL HUDAA

# HIJJA NA UMRAH KWA MUJIBU WA QUR'AN NA SUNNA

MTUNZI

LUQMAAN NASSOR ABDALLA BACHU

بسم الله الرحمن الرحيم

# الحج والعمرة على ضوء الكتاب والسنة

# HIJJA NA UMRA KWA MUJIBU WA QUR'AN NA SUNNAH

RIHLATUL HUDAA
HAJJ & UMRAH AGENCY

Mhariri: FARID SAID MOHAMMED, AL-AZKAWEY
Mhakiki: SAUDA ABDUL-MALIK SHAABAN, AL-BAAJUN

Mtunzi: LUQMAAN NASSOR ABDALLA BACHU

**YALIYOMO KATIKA KITABU**


SEHEMU YA KWANZA: UTANGULIZI ... 1
- Dibaji ... 1
- Umuhimu wa Hijja na Umra ... 2

SEHEMU YA PILI: MSINGI WA HIJJA NA UMRA ... 3
- Maana ya Hijja na Umra ... 3
- Hukumu ya Hijja na Umra ... 3
- Masharti ya Hijja na Umra ... 4
- Sharti la Ziada kwa Wanawake ... 4
- Uwajibu wa kutubia kutokana na maasi na dhulma ... 5
- Masharti ya Toba ya Kweli (Tawbah Nasuuha) ... 6

SEHEMU YA TATU: AINA ZA HIJJA ... 6

SEHEMU YA NNE: HATUA ZA UMRA ... 7
- Nguzo (Arkan) za Umra ... 7
- Wajibu (wajibat) za Umra ... 8
- Maana ya Sunnah: ... 8
- Baadhi ya sunnah ... 8
- Mambo yenye kuharibu ihram (Mahdhuuraat ) ... 9
- Miqat (المواقيت) ... 9
  - Maana ya Miqat: ... 9
  - Aina za Miqat: ... 10
- Ihram ya Umra (الإحرام) ... 13
  - Tawaf (الطواف) ... 14
  - Sa'yi (السعي) ... 17
  - Kunyoa au Kupunguza Nywele (الحلق أو التقصير) ... 18

SEHEMU YA TANO: HATUA ZA HIJJA ... 19
- NGUZO ZA HIJJA, WAJIBU NA SUNNAH ... 20
  - Nguzo za Hijja: ... 20
  - Wajibu za hijja (waajibaat) ... 20
  - Siku za Hijja ... 20

SEHEMU YA SITA: FIDIA NA UZUSHI ... 26
- Al-Fidya (الفدية) ... 26
- Uzushi na Makosa Yanayofanywa na Mahujaji ... 27

SEHEMU YA NANE: ZIYARA YA MASJID AL-NABAWI ... 29
- Hukumu ya Kutembelea Masjid al-Nabawi: ... 29
- Adabu za Ziyara: ... 30

MSIKITI WA QUBA NA FADHILA ZAKE ....................................................................32
SEHEMU YA TISA: MAS-ALA MUHIMU ..........................................................................33
Hijja kwa Niaba (الحج عن الغير): ..........................................................................................33
Hijja ya Mtoto Mdogo: ........................................................................................................34
Umra katika Ramadhani: .....................................................................................................34
SEHEMU YA KUMI: MAELEZO YA KINA KUHUSU HADIY NA UDHIYA.................34
Tofauti kati ya Hadiy na Udh-hiya: .......................................................................................34
MASWALI YANAYOULIZWA MARA KWA MARA.......................................................36
SEHEMU YA KUMI NA MOJA: HITIMISHO ....................................................................37

RIHLATUL HUDAA
HAJJ & UMRAH AGENCY

# SEHEMU YA KWANZA: UTANGULIZI

## Dibaji

Sifa zote njema anastahiki Allah, Mola wa walimwengu wote. Tunamshukuru, tunamuomba msaada, na tunamuomba msamaha. Tunajilinda kwake kutokana na shari za nafsi zetu na uovu wa matendo yetu. Yeyote anayeongozwa na Allah, hakuna wa kumpoteza, na yeyote anayepotezwa, hakuna wa kumwongoza.

Nashuhudia kwamba hakuna mungu anayestahiki kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah peke yake, hana mshirika. Na nashuhudia kwamba Muhammad ni mja wake na Mtume wake, rehema na amani ziwe juu yake, familia yake, maswahaba zake, na wote wanaowafuata kwa wema hadi siku ya Malipo.

Kitabu hiki kidogo ni mchango katika kuelezea ibada tukufu za Hijja na Umra kwa lugha ya Kiswahili, kwa kutegemea vyanzo vikuu vya Uislamu ambavyo ni Qur'an Tukufu na Sunnah sahihi ya Mtume Muhammad (ﷺ), kwa ufahamu wa wema waliotangulia (Salaf al-Salih). Lengo kuu ni kumsaidia msomaji, hasa anayezungumza Kiswahili, kuzifahamu ibada hizi kwa usahihi na kuepuka makosa na uzushi ambao umeenea miongoni mwa watu walio wengi.

Katika kuandaa kitabu hiki, nimezingatia sana vitabu viwili muhimu vya wanavyuoni wakubwa wa zama hizi (التحقيق والإيضاح لكثير من مسائل الحج والعمرة والزيارة) cha Sheikh Abdul Aziz bin Abdullah bin Baz (Allah amrehemu) na (دليل المعتبر) cha Sheikh Abu Yusuf bin Zabnillah bin Muhammad Al-Atir (Allah amhifadhi).

HAJJ & UMRAH AGENCY

Namuomba Allah Mtukufu akifanye kitabu hiki kiwe na manufaa kwa Waislamu, na akijaalie kuwa ni kazi iliyotakasika kwa ajili ya kutafuta radhi zake. Aamiin.

# Umuhimu wa Hijja na Umra



Hijja ni moja kati ya nguzo tano za Uislamu, na ni ibada muhimu sana katika maisha ya Muislamu. Umuhimu wake unadhihirika katika Qur'an na Sunnah. Allah Mtukufu anasema:

**وَلِلَّهِ عَلَى النَّاسِ حِجُّ الْبَيْتِ مَنِ اسْتَطَاعَ إِلَيْهِ سَبِيلًا ۚ وَمَن كَفَرَ فَإِنَّ اللَّهَ غَنِيٌّ عَنِ الْعَالَمِينَ**

“Na kwa ajili ya Allah ni wajibu kwa watu kuihiji Nyumba hiyo, kwa yule awezaye njia ya kwendea. Na atakayekanusha, basi hakika Allah ni Mkwasi, hahitaji walimwengu.” (Surat Al-Imran: 97)

Kadhalika, Mtume (ﷺ) amesisitiza umuhimu wa Hijja katika Hadith nyingi. Katika Hadith iliyopokewa na Ibn Umar (radhiyallahu anhuma), Mtume (ﷺ) amesema:

**بُنِيَ الإسْلامُ على خَمْسٍ: شَهادَةِ أنْ لا إلَهَ إلّا اللَّهُ وأنَّ مُحَمَّدًا رَسولُ اللَّهِ، وإقامِ الصَّلاةِ، وإيتاءِ الزَّكاةِ، والحَجِّ، وصَوْمِ رَمَضانَ.**

*[الراوي: عبدالله بن عمر • البخاري، صحيح البخاري (٨) • [صحيح] • أخرجه البخاري (٨) ، ومسلم. (١٦).]*

“Uislamu umejengwa juu ya mambo matano: Kushuhudia kwamba hakuna mungu anayestahiki kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah na kwamba Muhammad ni Mtume wa

Allah, kusimamisha Swala, kutoa Zaka, kuhiji Nyumba (Al-Kaaba), na kufunga Ramadhani." (Sahih Al-Bukhari: 8, Sahih Muslim: 16)

Fadhila za Hijja na Umra ni nyingi. Mtume (ﷺ) amesema:

**العُمْرَةُ إلى العُمْرَةِ كَفّارَةٌ لِما بيْنَهُما، والحَجُّ المَبْرُورُ ليسَ له جَزاءٌ إلّا الجَنَّةُ.**

*[الراوي: أبو هريرة • البخاري، صحيح البخاري (١٧٧٣) • [صحيح] • أخرجه البخاري (١٧٧٣) ، ومسلم (١٣٤٩)]*

"Umra moja hadi Umra nyingine ni kafara kwa yaliyo baina yao (madhambi), na Hijja iliyokubaliwa (Al-Hajj Al-Mabrur) haina malipo isipokuwa Pepo."
(Sahih Al-Bukhari: 1773, Sahih Muslim: 1349)

# SEHEMU YA PILI: MSINGI WA HIJJA NA UMRA

## Maana ya Hijja na Umra

- **Hijja (الحج):**

- **Kilugha:** Inamaanisha "kukusudia" kitu kitukufu.
- **Kisheria:** Ni kukusudia kwenda Makka kwa wakati maalum ili kutekeleza ibada maalum kwa masharti maalum.

- **Umra (العمرة):**

- **Kilugha:** Inamaanisha "kuzuru" au "kutembelea".
- **Kisheria:** Ni kukusudia kwenda Makka ili kutekeleza ibada maalum kwa masharti maalum bila kufungwa na wakati maalum.

HAJJ & UMRAH AGENCY

## Hukumu ya Hijja na Umra

- **Hukumu ya Hijja:** Hijja ni fardhi (wajibu) kwa kila Muislamu, mwanamume na mwanamke, ambaye ametimiza masharti yake, mara moja katika maisha. Ushahidi ni aya ya 97 ya Surat Al-Imran iliyotajwa hapo juu (Ukurasa nambari 2)

- **Hukumu ya Umra:** Wanachuoni wametofautiana kuhusu hukumu ya Umra. Wengine wamesema ni wajibu kama Hijja, na wengine wamesema ni Sunnah iliyosisitizwa. Kauli yenye nguvu ni kwamba Umra ni wajibu mara moja kwa mwenye uwezo, kwa dalili ya Hadith ya Aisha (radhiyallahu anha) alipomuuliza Mtume (ﷺ): "Ewe Mtume wa Allah, je, wanawake wana wajibu wa Jihad?" Akajibu: "Ndio, wana Jihad isiyo na mapigano: Hijja na Umra." (Imepokelewa na Imam Ahmad na Ibn Majah kwa sanad sahihi).

## Masharti ya Hijja na Umra

Ili Hijja na Umra ziwe wajibu kwa mtu (Mwanamme na Mwanamke), anapaswa kutimiza masharti yafuatayo:

1. **Uislamu:** Si wajibu kwa asiyekuwa muislamu.
2. **Akili:** Si wajibu kwa mwendawazimu.
3. **Baleghe:** Si wajibu kwa mtoto mdogo, lakini akihiji, Hijja yake ni sahihi na atapata thawabu, haitamuondolea wajibu wa Hijja ya Uislamu atakapofikia baleghe.
4. **Uhuru:** Si wajibu kwa mtumwa.
5. **Uwezo (الاستطاعة):** Hili ni sharti muhimu sana, na linajumuisha uwezo wa kimwili na kifedha (ikiwemo kuwacha gharama za familia uliyoiwacha nyuma) pamoja na amani ya njia. Allah anasema: "...kwa yule awezaye njia ya kwendea." (Surat Al-Imran: 97).

## Sharti la Ziada kwa Wanawake

**Mahram:** Mwanamke anapaswa kusafiri na mume wake au mahram wake (wanaume ambao ni haramu kwake kumuoa). Hii ni kwa mujibu wa Hadith ya Mtume (ﷺ): "Mwanamke asisafiri isipokuwa na mahram." (Sahih Al-Bukhari: 1862).

RIHLATUL HUDAA
HAJJ & UMRAH AGENCY

Lakini wanavyuoni wameeleza hali za dharura (الضرورة) na haja (الحاجة) ambazo zinaweza kumruhusu mwanamke kusafiri bila ya mahram, miongoni mwazo ni Hijja na Umra.

Imam Malik na baadhi ya Shaafii'yyah wameruhusu mwanamke kusafiri kwa Hija ya faradhi akiwa ana wanawake waaminifu pamoja nae na njia ni salama.

وَلَيْسَ المَحْرَمُ لِلمَرْأَةِ مِنَ الاسْتِطَاعَةِ، فَإِنْ وُجِدَ رِفْقَةٌ مَأْمُونَةٌ لَزِمَهَا الحَجُّ، رِجَالًا كَانُوا أَوْ نِسَاءً.

"Na haikuwa, kuwa na Mahram kwa mwanamke ni sharti la uwezo (uwezo wa yeye kuiendea hija), ikiwa atapata msafara wenye kuaminika (uaminifu) itamlazimikia yeye hija, iwe ni wanaume au wanawake. At-Talqin cha Abdul-Wahhab (Juzu 1/ uk. 200-202).

Pia kauli kama hiyo imekuja katika kitabu "Bidāyatul Mujtahid wa Nihāyatul Muqtasid" cha Ibn Rashid Al-hafiyd;

هَلْ مِنْ شَرْطِ وُجُوبِ الْحَجِّ عَلَى الْمَرْأَةِ أَنْ يَكُونَ مَعَهَا زَوْجٌ أَوْ ذُو مَحْرَمٍ مِنْهَا يُطَاوِعُهَا عَلَى الْخُرُوجِ مَعَهَا إِلَى السَّفَرِ لِلْحَجِّ؟

Je ni katika masharti ya kuwajibikiwa Hija mwanamke anatakiwa awe na mumewe au mahram yake?

فَقَالَ مَالِكٌ وَالشَّافِعِيُّ: لَيْسَ مِنْ شَرْطِ الْوُجُوبِ ذَلِكَ، وَتَخْرُجُ الْمَرْأَةُ إِلَى الْحَجِّ إِذَا وَجَدَتْ رُفْقَةً مَأْمُونَةً.

Malik na Shafii wakasema: "Hili si miongoni mwa masharti ya kuwa Hija ni wajibu, na mwanamke anaweza kutoka kwenda Hija iwapo atapata msafara wa salama na kuaminika (Juzuu 1 / uk 86-87).

Na yamekuja maelezo mingi ya wanavyuoni juu ya kujuzu mwanamke kusafiri safari ya Hija ya faradhi bila mahram kama alivyoeleza Sheikh Al Islaam ibn Taymiyya akinukuliwa na Ibn Muflih katika kitabu ( Al-Furuu` 3/236) na akaeleza sio Hija tu bali kila safari ya Twa'a (kumtii Allah).

## Uwajibu wa kutubia kutokana na maasi na dhulma.

Allah amewajibisha toba ya kweli kila wakati na kila hali hasahasa kabla ya kwenda Hijja au Umra, ili mtu asiende kwenye ibada tukufu akiwa na madhambi na haki za watu.

Allah anasema katika kitabu chake kitukufu:

RIHLATUL HUDAA
HAJJ & UMRAH AGENCY

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا تُوبُوا إِلَى اللَّهِ تَوْبَةً نَصُوحًا.

"Enyi mlioamini! Mtubieni Allah toba ya kweli." (Surah At-Tahrim, 66:8)

إِنَّ اللَّهَ يَأْمُرُ بِالْعَدْلِ وَالْإِحْسَانِ... وَيَنْهَى عَنِ الْفَحْشَاءِ وَالْمُنكَرِ وَالْبَغْيِ.

"Hakika Allah anaamrisha uadilifu na ihsani… na anakataza mambo machafu, maovu na dhulma."

(Surah An-Nahl, 16:90)

Na Mtume (ﷺ) anasema:

التَّائِبُ مِنَ الذَّنبِ كَمَن لَا ذَنبَ لَهُ

"Anayetubu dhambi ni kama asiye na dhambi."

(Ibn Majah)

اتَّقُوا الظُّلْمَ، فَإِنَّ الظُّلْمَ ظُلُمَاتٌ يَومَ القِيَامَةِ

"Jiepusheni na dhulma, kwani dhulma ni giza Siku ya Kiyama."

(Muslim)

## Masharti ya Toba ya Kweli (Tawbah Nasuuha)

1. Kuacha kufanya dhambi hilo mara moja.
2. Kujuta kwa dhati juu ya kosa lililopita.
3. Kuazimia kwa moyo kutorudia tena dhambi hilo.
4. Na ikiwa toba inahusu dhuluma kwa watu katika mali, heshima au uhai, basi huongezeka sharti la nne ambalo ni:
   Kumrejeshea mwenye haki haki yake, au kumuomba msamaha na kuridhiana naye.

Hivyo kupata Hijja iliyokubaliwa (mabrur) kunahitaji Tawbah ya kweli na moyo uliosafishwa na toba hiyo.

# SEHEMU YA TATU: AINA ZA HIJJA

Kuna aina tatu za kutekeleza ibada ya Hijja, na Muislamu anaweza kuchagua yoyote kati ya hizi:

1. **At-Tamattu' (التمتع):** Hii ni aina bora zaidi. Mtu anahirimia kwa ajili ya Umra pekee katika miezi ya Hijja. Anapofika Makka, anafanya Tawaf, Sa'yi, na kunyoa au kupunguza nywele, na hivyo anakuwa ametoka katika Ihram. Siku ya nane ya Dhul-Hijja (Yaumul Tarwiya), anahirimia tena kwa ajili ya Hijja na anatekeleza matendo yote ya Hijja. Mwenye kufanya Tamattu' anawajibika kuchinja mnyama (Hadyi).

2. **Al-Qiran (القران):** Mtu anahirimia kwa ajili ya Umra na Hijja pamoja. Anatekeleza matendo ya Hijja, na matendo ya Umra yanaingia ndani ya matendo ya Hijja. Atabaki

RIHLATUL HUDAA HAJJ & UMRAH AGENCY

katika Ihram yake hadi atakapomaliza matendo ya Hijja siku ya Eid. Mwenye kufanya Qiran pia anawajibika kuchinja mnyama (Hadyi).

3. **Al-Ifrad (الإفراد):** Mtu anahirimia kwa ajili ya Hijja pekee. Atabaki katika Ihram yake hadi atakapomaliza matendo ya Hijja siku ya Eid. Mwenye kufanya Ifrad hawajibiki kuchinja mnyama, lakini ni Sunnah kwake kufanya hivyo.

**Aina Bora Zaidi:** Aina bora zaidi ni **At-Tamattu'**, kwa sababu ndiyo aina aliyoamrisha Mtume (ﷺ) na akaitamani kwa maswahaba zake. Pia, inampa wepesi anayehiji kwa kumpa fursa ya kutoka katika Ihram kati ya Umra na Hijja.

# SEHEMU YA NNE: HATUA ZA UMRA

Ibada ya Umra ina nguzo na wajibu ambazo zinakamilisha utekelezaji wake. Hatua zake kwa ufupi ni kama ifuatavyo: kuingia katika Ihram (Nia), kutoka kwenye Miqat, kufanya Tawaf (kuzunguka Al-Kaaba), kufanya Sa'yi baina ya Swafa na Marwa, na kumalizia kwa kunyoa au kupunguza nywele.

- **Maana ya Nguzo (Rukn):** Nguzo ni tendo ambalo ibada haisihi (haikubaliki) bila ya kulitekeleza. Kuacha nguzo kwa kusahau au kwa makusudi hufanya ibada iwe batili, na hakuna fidia (damu) inayoweza kulifidia. Ni lazima kurudi na kutekeleza nguzo hiyo ili ibada ikamilike.

## Nguzo (Arkan) za Umra

1. **Ihram (الإحرام):** Ni nia ya kuingia katika ibada.
2. **Tawaf (الطواف):** Kuizunguka Al-Kaaba mara saba.
3. **Sa'yi (السعي):** Kutembea baina ya Swafa na Marwa mara saba

- **Maana ya Wajib (Wajibu):** Wajib ni tendo ambalo ni lazima litekelezwe. Anayeliacha kwa makusudi anapata dhambi, na anayeliacha kwa kusahau au kutokujua anawajibika kulifidia kwa kuchinja mnyama (Fidya/Damu), na ibada yake inakuwa sahihi.

RIHLATUL HUDAA
HAJJ & UMRAH AGENCY

## Wajibu (wajibat) za Umra

1. **Kuhirimia kutoka kwenye Miqat** (eneo maalum lililowekwa na sheria) au kutoka nje ya viunga vya haram kwa alie ndani ya Makkah.
2. **Kunyoa au Kupunguza Nywele**, kupunguza kadiri ya ncha ya kidole kwa mwanamke.

## Maana ya Sunnah:

Sunna ni yale mambo, kauli au vitendo vya Mtume (ﷺ) ambavyo si wajibu (lazima) lakina anaefanya hupata thawabu na asiefanya hapati dhambi, na ibada yake bado ni sahihi na hawajibiki kutoa fidia, kwani atakaekuja na sunnah basi kafanya jambo zuri zaidi.

## Baadhi ya sunnah

1. Kuoga (Ghusl/josho kubwa) kabla ya Ihram.
2. Kujitia manukato mwilini (wanaume tu na si kwenye nguo za ihram)
3. Mwanaume kuvaa nguo mbili nyeupe.
4. Kuleta Talbiya kwa sauti kuanzia Ihram ḥadi kuanza Tawaf (Wanaume tu ndio wanapaswa kudhihirisha sauti).
5. Kudumu na dhikri na dua njiani
6. Kukoga kabla kuingia Makka
7. Kutembea kwa haraka *(Ar-Raml*) katika mizunguko mitatu ya kwanza ya Tawaf ya kuingia (Wanaume tu).
8. Kufunua bega la kulia (*Al-Idhtibaa')* katika Tawaf ya kuingia.
9. Kubusu Hajarul-Aswad, kugusa kwa mkono wa kulia endapo itawezekana au kuashiria.
10. Kuswali rakaa mbili nyuma ya Maqam Ibrahim baada ya Tawaf.
11. Kunywa maji ya Zamzam.
12. Kukimbia kidogo baina ya alama za kijani wakati wa Sa'yi (kwa wanaume).

RIHLATUL HUDAA
HAJJ & UMRAH AGENCY

## Mambo yenye kuharibu ihram (Mahdhuuraat )


1. Kuondoa nywele kichwani au sehemu yoyote ya mwili.
2. Kukata kucha.
3. Kujitia manukato baada ya ihram (nia).
4. Kufunika kichwa kwakitu chenye kugandamana na kichwa kama kofia,kilemba au vazi lenyewe la ihram (wanaume).
5. Kuvaa nguo iliyoshonwa kama suruali,shati,kanzu (wanaume).
6. Kuvaa niqabu na glovu (gloves) kwa mwanamke.
7. Kukumbatia,kutizama au kubusu kwa matamanio.
8. Kufanya jimai.
9. Kuwinda na kuuwa wanyama.
10. Kuuwa wanyama wa haram au kuwafukuza.
11. Kufunga ndoa, kuposa au kumposea mwengine.
12. Kuvaa viatu vinavyozidi vifundo vya miguu (wanaume)

## Miqat (المواقيت)

### Maana ya Miqat:

- **Kilugha:** Ni neno la Kiarabu linalomaanisha "mipaka" au "sehemu zilizowekwa".
- **Kisheria:** Ni mipaka ya kijiografia (Miqat Makani) na mipaka ya wakati (Miqat Zamani) ambayo imewekwa na Sharia kwa ajili ya anayekusudia kufanya Hijja au Umra.

RIHLATUL HUDAA
HAJJ & UMRAH AGENCY




## Aina za Miqat:

1. **Miqat za Wakati (المواقيت الزمانية):** Hii ni mipaka ya muda ambayo ndani yake ndipo ibada ya Hijja hufanywa. Allah anasema:

الْحَجُّ أَشْهُرٌ مَّعْلُومَاتٌ.

"Hijja ni miezi maalumu." (Surat Al-Baqarah: 197)

Miezi hiyo ni Shawwal, Dhul-Qa'dah, na siku kumi za mwanzo za Dhul-Hijjah. Ama Umra, haina wakati maalum, inaweza kufanywa wakati wowote ule katika mwaka.

2. **Miqat za Mahali (المواقيت المكانية):** Hii ni mipaka ya kijiografia ambayo Mtume (ﷺ) aliwawekea watu wanaokusudia kuhiji au kufanya Umra. Mtu haruhusiwi kuivuka mipaka hii kuelekea Makka bila kuingia katika hali ya Ihram. Mipaka hiyo ni kama ifuatavyo:

| **Jina la Miqat** | **Eneo Lake** | **Watu Wanaohusika** |
|---|---|---|
| **Dhul-Hulayfah** | Kusini mwa Madina (takriban km 450 kutoka Makka) | Watu wa Madina na wanaopitia njia hiyo. |

| Jina la Miqat | Eneo Lake | Watu Wanaohusika |
|---|---|---|
| **Al-Juhfah** | Karibu na mji wa Rabigh (takriban km 183 kutoka Makka) | Watu wa Sham (Syria, Jordan, Palestina) na Misri (Egypt) na wanaopita njia hiyo. |
| **Qarnul-Manazil** | Karibu na Taif (takriban km 75 kutoka Makka) | Watu wa Najd (Riyadh na maeneo ya kati ya Saudi Arabia) na wanaopita njia hiyo. |
| **Yalamlam** | Kusini mwa Makka (takriban km 92 kutoka Makka) | Watu wa Yemen na wanaopitia njia hiyo. |
| **Dhatu 'Irq** | Kaskazini-mashariki mwa Makka (takriban km 94 kutoka Makka) | Watu wa Iraq na Iran na wanaopita njia hiyo. |

**إنَّ النبيَّ ﷺ وقَّتَ لأهْلِ المَدِينَةِ ذا الحُلَيْفَةِ، ولِأَهْلِ الشَّأْمِ الجُحْفَةَ، ولِأَهْلِ نَجْدٍ قَرْنَ المَنازِلِ، ولِأَهْلِ اليَمَنِ يَلَمْلَمَ، هُنَّ لهنَّ، - ولِمَن أتى عليهنَّ مِن غيرِهِنَّ مِمَّنْ أرادَ الحَجَّ والعُمْرَةَ، ومَن كانَ دُونَ ذلكَ، فَمِنْ حَيْثُ أنْشَأَ حتَّى أهْلُ مَكَّةَ مِن مَكَّةَ.**

الراوي: عبدالله بن عباس • البخاري، صحيح البخاري (١٥٢٤) • [صحيح] • أخرجه مسلم (١١٨١)

"Hakika Mtume ﷺ aliwawekea watu wa Madina Dhul-Hulayfah (kama miiqat), na kwa watu wa Shamu Al-Juhfah, na kwa watu wa Najd Qarn al-Manazil, na kwa watu wa Yemen Yalamlam. Mipaka hii ni kwa ajili ya watu wa maeneo hayo na kwa yeyote atakayepitia humo kutoka maeneo mengine akiwa na nia ya kuhiji (Hajj) au kufanya Umra. Na yule ambaye yuko karibu zaidi (na Makkah kuliko mipaka hiyo), basi atahirimia kutoka pale alipoanzia safari yake, hata watu wa Makkah watahirimia kutoka Makkah."

Imepokelewa na Al-Bukhari katika Sahih al-Bukhari (hadithi namba 1524) Pia imepokewa na: Muslim (hadithi namba 1181).

**Hukumu ya Kupita Miqat Bila Ihram:** Mtu anayekusudia Hijja au Umra haruhusiwi kuivuka Miqat bila kuingia katika Ihram (Nia). Ikiwa ataivuka kimakusudi bila Ihram, anawajibika kurudi kwenye Miqat na kuhirimia hapo. Ikiwa hataweza kurudi, anawajibika kuchinja mnyama (Fidya) huko Makka na kuwagawia masikini.

**Hukumu ya Kupita Miqat kwa njia ya anga (Ndege):** Msafiri anaweza kuvaa nguo za ihram akiwa nyumbani au uwanja wa ndege kabla ya kupanda ndege. Hata hivyo nia ya kuingia katika ihram inapaswa kunuwiwa wakati ndege inapokaribia au inapokuwa sambamba na Miqat. Kwa kawaida marubani na wahudumu hutangaza wakati huu unapowadia. Hivyo mwenye kukusudia Hijja au Umra atahirimia juu ya ndege wakati wa kupita Miqat (kituo cha kuhirimia).

**Nini cha Kufanya Ukipita Miqat Bila Ihram**

Kuna hali mbili kuu zinazoweza kutokea:

1. Kupita kwa Kusahau

   Ikiwa mtu atapita Miqat bila kuingia ihram (nia) kwa sababu ya kusahau, hakuna dhambi juu yake, kwa kuwa Allah anasamehe makosa yanayotokana na kusahau. Hata hivyo, anapaswa kuchukua hatua zifuatazo:

   a. Kurudi kwenye Miqat: Anapaswa kurudi kwenye Miqat na kuhirimia kutoka hapo. Akifanya hivyo, hakuna fidia (damu) inayomlazimu, kwa mujibu wa makubaliano ya wanazuoni.

   b. Kutokurudi kwenye Miqat: Ikiwa hatarudi kwenye Miqat na akahirimia kutoka mahali alipo (kama vile Jeddah), basi anawajibika kutoa fidia (damu), ambayo ni kuchinja mnyama (kondoo au mbuzi) huko Makkah na kuwagawia masikini.

2. Kupita kwa Kukusudia

   Ikiwa mtu atapita Miqat kwa makusudi bila kuingia ihram, anapata dhambi na anawajibika kutoa fidia (damu), hata kama atarudi kwenye Miqat na kuhirimia kutoka hapo. Hii ni kwa sababu amevunja amri ya Sharia kwa kukusudia.

RIHLATUL HUDA
HAJJ & UMRAH AGENCY

Mwenye kuhiji au kufanya Umra atalazimika kufanya mambo yafuatayo atakapofika Miiqaat:

## Ihram ya Umra (الإحرام)

**Maana ya Ihram:** Ni nia ya kuingia katika ibada ya Hijja au Umra. Pindi Muislamu anaponuia na kuanza Talbiya, anakuwa ameingia katika hali ya Ihram na hivyo anajizuia na mambo yaliyoharamishwa (Mahdhuuraat).

**Jinsi ya Kuingia Katika Ihram:** Ni Sunnah kwa anayetaka kuhirimia kufanya yafuatayo kabla ya kunuia:

1. Kukata kucha, kunyoa nywele za kwapani na sehemu za siri.
2. Kuoga Ghusl (Josho kubwa), kama ilivyothibiti kutoka kwa Mtume (ﷺ).
3. Mwanamume kujipaka manukato (attar) mwilini mwake, lakini si kwenye nguo za Ihram.
4. Mwanamume kuvaa nguo mbili nyeupe, zisizo na mshono Izar na Ridaa (Shuka mbili nyeupe ya chini na ya juu). Ama mwanamke, atavaa nguo yoyote anayotaka bila kuainisha rangi maalumu, yenye kusitiri mwili wake mzima isipokuwa kufunika uso kwa niqab na kuvaa glavu.

**TANBIHI:**

Ikiwa atapita katika Kundi la wanaume, atafanya kama alivoeleza Mama Aisha (radhi za Allah ziwe juu yake:

**عَنْ عَائِشَةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهَا قَالَتْ : كَانَ الرُّكْبَانُ يَمُرُّونَ بِنَا وَنَحْنُ مَعَ رَسُولِ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ مُحْرِمَاتٌ ، فَإِذَا حَاذَوْا بِنَا سَدَلَتْ إِحْدَانَا جِلْبَابَهَا مِنْ رَأْسِهَا عَلَى وَجْهِهَا ، فَإِذَا جَاوَزُونَا كَشَفْنَاهُ.**

Kutoka kwa Aisha (radhi za Allah ziwe juu yake) amesema: "Wasafiri (wanaume waliopanda wanyama) walikuwa wakitupita hali ya kuwa tuko na Mtume wa Allah ﷺ katika ihram. Walipokuwa wakitukaribia, mmoja wetu alikuwa akiteremsha jilbab (vazi lake la juu) kutoka kichwani mwake na kuufunika uso wake. Na walipotupita, tulikuwa tukiufunua."
(Imepokewa na Imam Ahmad, Abu Daud, na Ibn Majah).

Hivyo mwanamke ataruhusiwa kufunika usowake kwenye kundi la wanaume kwasababu asili mwanamke haruhusiwi kuonekanwa chochote na mwanaume ambae si mahram yake.

5. Kuswali Swala ya faradhi ikiwa wakati wake umefika (miqat), au kuswali rakaa mbili za Sunnah ya vazi la ihraam.

Baada ya hayo, ananuia kuingia katika Umra kwa kusema:

**Labbayka Umratan (لَبَّيْكَ عُمْرَةً)**

Ama;

**Labbayka Allahumma Umratan (لَبَّيْكَ اللَّهُمَّ عُمْرَةً)**

Kisha anaanza kuleta Talbiya.

**Talbiya (التلبية):** Talbiya ni kauli anayoitamka anayehiji au kufanya Umra. Mtume (ﷺ) alikuwa akisema:

لَبَّيْكَ اللَّهُمَّ لَبَّيْكَ، لَبَّيْكَ لَا شَرِيكَ لَكَ لَبَّيْكَ، إِنَّ الْحَمْدَ وَالنِّعْمَةَ لَكَ وَالْمُلْكَ، لَا شَرِيكَ لَكَ

Labbayka Allāhumma labbayk, labbayka lā sharīka laka labbayk, innal-ḥamda wan-ni'mata laka wal-mulk, lā sharīka lak.

"Nimeitika wito wako, Ewe Mwenyezi Mungu, nimeitika. Nimeitika, huna mshirika, nimeitika. Hakika sifa njema na neema ni zako na ufalme ni wako. Huna mshirika."
(Sahih Al-Bukhari: 1549)

Mtu ataendelea kuleta Talbiya kwa sauti (wanaume) hadi atakapoliona Al-Kaabah kwa ajili ya kuanza Tawaf, wanawake hawatodhihirisha sauti zao (kwa kadri ya kujiskia mwenyewe).

RIHLATUL HUDAA
HAJJ & UMRAH AGENCY

## Tawaf (الطواف)

**Maana ya Tawaf:** Ni kuizunguka Al-Kaaba mara saba kwa nia ya ibada.

**Masharti ya Tawaf:**

1. **Nia:** Kukusudia kufanya Tawaf.
2. **Tohara:** Kuwa msafi kutokana na hadathi ndogo na kubwa (kuwa na udhu).
3. **Kusitiri Uchi:** Kuvaa nguo zinazositiri uchi.

4. **Kuanzia Hajarul-Aswad:** Kuanza mzunguko kwenye pembe ya Hajarul-Aswad (Jiwe jeusi).
5. **Al-Kaaba Kushotoni:** Kuifanya Al-Kaaba iwe upande wake wa kushoto wakati wote wa kuzunguka.
6. **Kuzunguka Nje ya Al-Kaaba:** Tawaf ifanyike nje ya eneo la Hijr Ismail (Baadhi ya wanavyuoni wanaona kuwa ni makosa kuita hijr Ismail, usawa ni Hijr).
7. **Kukamilisha Mizunguko Saba:** Kukamilisha mizunguko yote saba.

**Jinsi ya Kufanya Tawaf:**

1. Anapoingia Masjid Al-Haram baada ya kuliona Kaaba, ataacha kuleta Talbiya na kuelekea kwenye Hajarul-Aswad.
2. Ataibusu Hajarul-Aswad ikiwezekana, au kuigusa kwa mkono wa kulia na kuubusu mkono, au kuielekezea ishara kwa mbali na kusema "Bismillah Allahu Akbar".
3. Ataanza mzunguko wa kwanza, akitembea haraka kidogo (Ar-Raml) katika mizunguko mitatu ya mwanzo (kwa wanaume ikiwezekana hivyo).
4. Mzunguko utaanza kwenye jiwe jeusi na kumaliza kwenye jiwe jeusi, hapo atahisabika amekamilisha mzunguko wa kwanza, nakadhalika iliyobakia.
5. Katika mizinguko yote ya Tawaf, Atakithirisha dhikri, kumswalia mtume na dua kwa wingi.
6. Akifika kwenye jiwe jiusi kwaajili ya mzunguko wa pili na inayofuata atasema “Allahu Akbar” nasio kama alivosema wakati alipoanza mzunguko wa kwanza“Bismillah  Allahu Akbar” hii ni kwa mzunguko wa mwanzo tu.
7. Katika Tawaf hii ya Umra, ni Sunnah kwa mwanamume kufanya Al-Idhtibaa', yaani kufunua bega la kulia na kulifunika la kushoto (Rubega).
8. Kila anapofika kwenye pembe ya Yemeni (Ar-Rukn Al-Yamani), ataigusa ikiwezekana bila kuibusu.
9. Baina ya pembe ya Yemeni na Hajarul-Aswad, atasoma dua:

رَبَّنَا آتِنَا فِي الدُّنْيَا حَسَنَةً وَفِي الْآخِرَةِ حَسَنَةً وَقِنَا عَذَابَ النَّارِ.

Rabbana atina fid-dunya hasanatan wa fil-ākhirati hasanatan waqinā ‘adhāban-nār.

"Mola wetu, tupe duniani mema, na Akhera mema, na utulinde na adhabu ya Moto."
(Surat Al-Baqarah: 201)

10. Atakamilisha mizunguko saba kwa namna hiyo. Baada ya kumaliza, ataelekea nyuma ya Maqam Ibrahim huku akisoma:

وَاتَّخِذُوا مِن مَّقَامِ إِبْرَاهِيمَ مُصَلًّى


"na fanyeni sehemu ya kusimama Ibrahim kuwa ni mahali pa kusalia (kuswali.)"

Kuswali rakaa mbili; Rakaa ya kwanza atasoma suratul fatiha pamoja na suratul kaafiruun, rakaa ya pili suratul fatiha pamoja na suratul ikhlaas (sunnah kusoma surah hizo akipenda atasoma zozote).

11. Atakwenda kunywa maji ya zamzam na ataomba dua pamoja na kujipaka usoni na kichwani. Mtume (ﷺ) anasema: «مَاءُ زَمْزَمَ لِمَا شُرِبَ لَهُ»

"Maji ya Zamzam ni kwa (huleta manufaa kulingana na) kile mtu anachokinywea (anachokusudia kwa dua)"

!!! Wanawake wajichunge kujirowesha nguo zao zisije zikasifia maumbo yao!!!.



## Sa'yi (السعي)

**Maana ya Sa'yi:** Ni kutembea baina ya vilima viwili vya Swafa na Marwa mara saba

**Jinsi ya Kufanya Sa'yi:**

1. Baada ya kuswali rakaa mbili za Tawaf, ataelekea kwenye kilima cha Swafa na anapokaribia Swafa atasema

   ‘ Abda’u bimā bada’a Allāhu bihi’ " أَبْدَأُ بِمَا بَدَأَ اللَّهُ بِهِ " (“Naanza kwa kile ambacho Mwenyezi Mungu alianza nacho).

   Kisha atasoma:

إِنَّ ٱلصَّفَا وَٱلْمَرْوَةَ مِن شَعَآئِرِ ٱللَّهِۖ فَمَنْ حَجَّ ٱلْبَيْتَ أَوِ ٱعْتَمَرَ فَلَا جُنَاحَ عَلَيْهِ أَن يَطَّوَّفَ بِهِمَاۚ وَمَن تَطَوَّعَ خَيْرًا فَإِنَّ ٱللَّهَ شَاكِرٌ عَلِيمٌ

“Hakika vilima vya Safaa na Marwa ni katika alama za Allah. Basi anaye hiji kwenye Nyumba hiyo au akafanya Umra, si kosa kwake kuvizunguka. Na anaye jitendea kheri mwenyewe, basi bila ya shaka Allah ni mwenye shukrani na Mjuzi.”
(Surat Al-Baqarah: 158)

2. Atapanda juu ya kilima cha Swafa, ataelekea Al-Kaaba (kibla), atainua mikono na kumsifu Allah na ataleta dhikri ifuatayo Atasema:


**لَا إِلٰهَ إِلَّا اللهُ، وَحْدَهُ لَا شَرِيكَ لَهُ، لَهُ الْمُلْكُ، وَلَهُ الْحَمْدُ، يُحْيِي وَيُمِيتُ، وَهُوَ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ قَدِير.**
**لَا إِلٰهَ إِلَّا اللهُ وَحْدَهُ، أَنْجَزَ وَعْدَهُ، وَنَصَرَ عَبْدَهُ، وَهَزَمَ الْأَحْزَابَ وَحْدَهُ.**

"La ilaha illa Allah wahdahu la sharika lah, lahul-mulku wa lahul-hamdu, yuhyi wa yumiit, wa huwa 'ala kulli shay'in qadir. La ilaha illa Allah wahdah, anjaza wa'dah, wa nasara 'abdah, wa hazamal-ahzaba wahdah."

Kisha ataomba dua anayoitaka, kisha atarejea iyo dhikri kwa mara ya pili, alafu ataomba dua tena kwa mara ya pili, kisha atarejea dhikri kwa mara ya tatu kisha hatoomba dua ataelekea marwa (dhikri mara tatu (3) na dua mara (2)).

RIHLATUL HUDAA
HAJJ & UMRAH AGENCY

3. Kisha atateremka na kuelekea Marwa. Katikati ya njia, kuna eneo lililowekwa alama za taa za kijani. Katika eneo hili, ni Sunnah kwa wanaume kukimbia kidogo.
4. Anapofika Marwa, atapanda juu yake, ataelekea Qibla, na kufanya kama alivyofanya Swafa. Huu unakuwa ni mzunguko wa kwanza.
5. Atarudi tena kuelekea Swafa, na huu utakuwa mzunguko wa pili. Ataendelea hivyo hadi atakapokamilisha mizunguko saba, akianzia Swafa na kumalizia Marwa.
6. Baina ya safa na marwa atakithirisha kumtaja Allah sana na dhikri nyengine mbali mbali pamoja na kukithirisha dua, kumswalia mtume kwa wingi na bora ya dhikri kuliko zote ni kusoma Qur an.




RIHLATUL HUDAA
HAJJ & UMRAH AGENCY


## Kunyoa au Kupunguza Nywele (الحلق أو التقصير)

Baada ya kumaliza Sa'yi, mwanaume atanyoa nywele zake zote (Al-Halq) au atazipunguza zote (At-Taqsir). Kunyoa zote ni bora zaidi, kwani Mtume (ﷺ) aliwaombea rehema mara tatu wale wanaonyoa zote. Mwanamke atapunguza nywele zake kidogo tu, kiasi cha ncha ya kidole.

Kwa kufanya hivi, mtu anakuwa amekamilisha ibada yake ya Umra na anakuwa ametoka katika hali ya Ihram (amehalalika), na hivyo anaruhusiwa kufanya yale yote yaliyokuwa haramu kwake wakati wa Ihram.

# SEHEMU YA TANO: HATUA ZA HIJJA

Ibada ya Hijja ni nguzo ya tano ya Uislamu na inahusisha mfululizo wa matendo matakatifu yanayofanywa katika mji wa Makka na maeneo yake ya jirani katika siku maalum za mwezi wa Dhul-Hijjah. Matendo haya huanza rasmi siku ya nane ya Dhul-Hijjah na kuendelea hadi siku ya kumi na tatu.



# NGUZO ZA HIJJA, WAJIBU NA SUNNAH

## Nguzo za Hijja:

1. **Ihram** – الدخول في الإحرام
2. **Kusimama Arafah** – الوقوف بعرفة
3. **Tawaf al-Ifadha** – طواف الإفاضة
4. **Sa'i** – السعي بين الصفا والمروة

## Wajibu za hijja (waajibaat)

1. Ihram (Nia) miqat zinazotambulikanwa kisheria.
2. Kusimama Arafa mpaka kuzama jua (kwa aliesimama mchana).
3. Kulala usiku Muzdalifa (usiku wa siku ya kuchinja).
4. Kulala usiku Mina katika siku za Tashriq.
5. Kurembea mawe Jamarat Al-Aqaba siku ya Eid na zilizobakia (3) ayam tashriq.
6. Kunyoa au kupunguza nywele.
7. Tawaf Al wadaa (tawaf yakuaga).

**Sunna za Hijja:**

Ama sunnah za hijja zinaingia sunnah zote za umra pamoja na Tawaf Al-qudum, kulala mina siku ya nane (8) na nyenginezo zisizokuwa nguzo na wajib.

## Siku za Hijja

Siku kumi za mwanzo za mwezi wa Dhul-Hijjah zina fadhila kubwa katika Uislamu. Mtume (ﷺ) amesema:

مَا مِنْ أَيَّامٍ الْعَمَلُ الصَّالِحُ فِيهِنَّ أَحَبُّ إِلَى اللَّهِ مِنْ هَذِهِ الْأَيَّامِ الْعَشْرِ.

"Hakuna siku ambazo matendo mema yanapendwa zaidi na Allah kuliko siku hizi kumi."
(Sahih Al-Bukhari: 969)

Katika siku hizi, Waislamu wanahimizwa kufanya matendo mema kama vile kufunga, kusoma Qur'an, kutoa sadaka, na kumdhukuru Allah kwa wingi.

## Yaumul Tarwiya (Siku ya 8 ya Dhul-Hijjah)

Hii ndiyo siku ambayo manasik (ibada) za Hijja huanza rasmi. Na imeitwa hivyo kwasababu zamani mahujaji walikua wakijiandaa na kwenda mina na kujaza maji kwaajili ya safari ya ibada.

1. **Kuhirimia:** Anayefanya Hijja ya Tamattu' (ambaye alikuwa ameshatoka kwenye Ihram yake baada ya Umra) atahirimia tena kwa ajili ya Hijja kutoka mahali alipo (Makka). Ni Sunnah kuoga, kujipaka manukato na kufanya kama alivyofanya miqat, na kisha kunuia Hijja akisema: **"لَبَّيْكَ حَجًّا" (Labbayka Hajjan)** Au; **" لَبَّيْكَ اللَّهُمَّ حَجّاً " (Labbayka llahumma Hajjan)**, kisha atakithirisha talbiya mpka atakaporembea mawe jamaratul akabah.

2. **Kwenda Mina:** Baada ya kuhirimia, mahujaji wote (wanaofanya Tamattu', Qiran, na Ifrad) wataelekea Mina, eneo liliopo kati ya Makka na Muzdalifa. Watabaki Mina siku hii yote na usiku wake.



3. **Sala Mina:** Wakiwa Mina, wataswali Swala za Dhuhr, Asr, Maghrib, na Isha, kila Swala kwa wakati wake, wakizipunguza Swala za rakaa nne (Dhuhr, Asr, Isha) kuwa rakaa mbili, bila kuzijumuisha (kuziswali pamoja).

## Yaumu Arafa (Siku ya 9 ya Dhul-Hijjah)

Hii ndiyo siku muhimu zaidi katika ibada ya Hijja. Ni nguzo kuu ya Hijja, na Hijja haikamiliki bila kusimama (Wuquf) katika uwanja wa Arafa. Mtume (ﷺ) amesema:

الْحَجُّ عَرَفَةُ.

"Hijja ni Arafa." (Sunan At-Tirmidhi: 889)



Viwanja vya Arafa, Mahali pa kusimama (Nguzo kuu ya Hijja)

1. **Kuondoka Mina:** Baada ya jua kuchomoza siku ya Arafa, mahujaji wataondoka Mina na kuelekea Arafa ni sunnah kufikia kwanza Namirah ikiwa litawezekana hilo kama alivofanya Mtume (ﷺ)... Khatibu hapo namira atakhutubia watu kulingana na hali na kuwabainishia yale yaliowajibu kwao siku ile (Arafa) na baada yake.

2. **Kisimamo Cha Arafa (Wuquf):** Watasimama katika uwanja wa Arafa. Wakati wa kisimamo huanza baada ya kupinduka kwa jua (baada ya Dhuhr) na unaendelea hadi kuzama kwa jua. Ni Sunnah kwa aliye Arafa kusimama akielekea Qibla, akiinua mikono yake na kuomba dua kwa wingi, akimdhukuru Allah, na kumswalia Mtume (ﷺ) pamoja na kusoma Qur'an.

3. **Swala Arafa:** Wataswali Swala za Dhuhr na Asr kwa kuzijumuisha na kuzipunguza (Jam'u Taqdim). Wataswali Dhuhr rakaa mbili na Asr rakaa mbili, kwa adhana moja

RIHLATUL HUDAA
HAJJ & UMRAH AGENCY

na iqama mbili.

4. **Dua ya Arafa:** Mtume (ﷺ) amesema: "Dua bora ni dua ya siku ya Arafa, na neno bora nililolisema mimi na Manabii kabla yangu ni:

**لا إله إلا الله وحده لا شريك له، له الملك وله الحمد وهو على كل شيء قدير**

(La ilaha illa Allah wahdahu la sharika lah, lahul-mulku wa lahul-hamdu, wa huwa 'ala kulli shay'in qadir)."

## Kuondoka Arafa na Kuelekea Muzdalifa

1. **Kuondoka Arafa:** Baada ya jua kuzama siku ya Arafa, mahujaji wataondoka Arafa na kuelekea Muzdalifa kwa utulivu na unyenyekevu na watakithirisha talbiya.

2. **Swala Muzdalifa:** Watakapofika Muzdalifa, wataswali Swala za Maghrib na Isha kwa kuzijumuisha na kuzipunguza (Jam'u Ta'khir). Wataswali Maghrib rakaa tatu na Isha rakaa mbili, kwa adhana moja na iqama mbili.

3. **Kulala Muzdalifa:** Watabaki Muzdalifa usiku kucha hadi alfajiri. Ni ruhusa kwa wanyonge (kama wagonjwa, wazee, na wanawake) kuondoka Muzdalifa baada ya nusu ya usiku na kuelekea mina.



4. **Kukusanya Mawe:** Ni Sunnah kukusanya mawe madogo (ukubwa wa punje ya kunde) kwa ajili ya kurusha Jamarat. Mtu atahitaji mawe 7 kwa ajili ya siku ya

kwanza (Yaumul Nahr) na mawe 21 kwa kila siku inayofuata (siku tatu; jumla mawe 70) ataokota mina.

### Yaumul Nahr (Siku ya 10 ya Dhul-Hijjah/ Siku ya Kuchinja)



Hii ni siku ya Eid al-Adha na ni siku yenye matendo mengi zaidi katika Hijja. Matendo ya siku hii ni manne:

1 **Kurusha Jamrat Al-Aqaba:** Baada ya kuswali Alfajiri Muzdalifa na kusimama kuelekea kibla kukithirisha dhikri na kuomba dua na inapendekezwa kuinua mikono, hadi mapambazuko, mahujaji wataelekea Mina. Wakifika kwenye Jamrat Al-Aqaba (nguzo kubwa) watakata talbiya na kuirushia kwa mawe saba, wakisema "Allahu Akbar" kwa kila jiwe.

RIHLATUL HUDAA
HAJJ & UMRAH AGENCY

2 **Kuchinja Mnyama (Hadyi):** Baada ya kurusha Jamarat, wale wanaofanya Hijja ya Tamattu' na Qiran watawajibika kuchinja mnyama wao. Ni Sunnah kula sehemu ya nyama hiyo na kuwagawia masikini.

3 **Kunyoa au Kupunguza Nywele:** Baada ya kuchinja, mwanaume atanyoa nywele zake zote (bora zaidi) au atazipunguza. Mwanamke atapunguza kidogo. Kwa kufanya

hivi, anakuwa amepata **Tahallul ya Kwanza**, ambapo anaruhusiwa kufanya kila kitu alichokatazwa wakati wa Ihram isipokuwa tendo la ndoa.

4 **Tawaf Al-Ifadha:** Baada ya hayo, atateremka kwenda Makka na kufanya Tawaf Al-Ifadha, ambayo ni nguzo ya Hijja. Kisha ataswali rakaa mbili nyuma ya Maqam Ibrahim. Baada ya Tawaf, atafanya Sa'yi baina ya Swafa na Marwa ikiwa anafanya Hijja ya Tamattu', au ikiwa hakufanya Sa'yi pamoja na Tawaf ya kuingia (Tawaf Al-Qudum) kwa wale wanaofanya Qiran na Ifrad. Baada ya kukamilisha Tawaf na Sa'yi, anakuwa amepata **Tahallul ya Pili**, na anaruhusiwa kufanya kila kitu, ikiwemo tendo la ndoa.

### Ayyamul Tashriq (Siku ya 11, 12, na 13 ya Dhul-Hijjah)

1. **Kukaa Mina:** Mahujaji watarudi Mina na kukaa huko kwa siku mbili au tatu.
2. **Kurusha Jamarat:** Kila siku baada ya kupinduka kwa jua, watarusha Jamarat tatu: Jamrat Al-Ula (ndogo), Jamrat Al-Wusta (ya kati), na Jamrat Al-Aqaba (kubwa). Kila moja itarushiwa kwa mawe saba. Ni Sunnah kusimama na kuomba dua baada ya kurusha Jamarat mbili za mwanzo.
3. **Kuondoka Mina:** Anayeruhusiwa ni yule anayetaka kufanya haraka (Ta'ajjul), anaweza kuondoka Mina siku ya 12 baada ya kurusha Jamarat na kabla ya jua kuzama. Anayebaki hadi siku ya 13 atarusha Jamarat siku hiyo pia, na hilo ndilo bora zaidi.

### Tawaf Al-Wada' (Tawaf ya Kuaga)

Kabla ya kuondoka Makka, tendo la mwisho ambalo mahujaji wanapaswa kufanya ni Tawaf Al-Wada' (Tawaf ya Kuaga). Ni wajibu kwa mujibu wa kauli yenye nguvu ya wanachuoni, isipokuwa kwa mwanamke aliye katika hedhi au nifasi. Baada ya Tawaf hii, mtu anapaswa kuondoka Makka moja kwa moja.

KIHLUL HUDAA
HAJJ & UMRAH AGENCY

**Tofauti kati ya Hijja na Umra:**

| Kigezo | Hijja | Umra |
|---|---|---|
| **Wakati** | Ina wakati maalum (Miezi ya Hijja: Shawwal, Dhul-qaada na siku 10 za Dhul-Hijja) | Inaweza kufanywa wakati wowote wa mwaka |
| **Hukumu** | Fardhi (wajibu) mara moja kwa mwenye uwezo | Wajibu au Sunnah (kuna ikhtilafu) |
| **Nguzo** | Ina nguzo nne, ikiwemo kusimama Arafa | Nguzo zake ni tatu (Ihram, Tawaf, Sa'yi) |
| **Ukamilifu** | Ni ibada ndefu na ngumu zaidi | Ni ibada fupi na rahisi zaidi |

# SEHEMU YA SITA: FIDIA NA UZUSHI

## Al-Fidya (الفدية)

Fidya ni malipo anayotoa mtu kwa kuacha wajibu au kwa kufanya jambo lililokatazwa katika Ihram. Aina za fidia hutofautiana kulingana na kosa lenyewe.

1. **Kwa kuacha Wajibu (kama kulala Muzdalifa au kurusha Jamarat):** Fidia yake ni kuchinja mbuzi au kondoo mmoja huko Makka na kuwagawia masikini.
2. **Kwa kufanya Mahdhurat (kama kunyoa, kuvaa nguo za kushonwa, kujipaka manukato):** Mtu anapewa hiari kati ya mambo matatu:
    a. Kuchinja mbuzi/kondoo.
    b. Kufunga siku tatu.
    c. Kulisha masikini sita, kila mmoja nusu ya pishi (kama kilo 1.5) ya chakula.
3. **Kwa kuwinda:** Fidia yake ni kuchinja mnyama anayefanana na yule aliyemwinda, au kutoa thamani yake kama chakula kwa masikini, au kufunga.
4. **Kwa kufanya tendo la ndoa (Jimaa):**
    a. **Kabla ya Tahallul ya Kwanza:** Hili huharibu Hijja. Mhusika atawajibika kuendelea na matendo yote ya Hijja iliyoharibika, kuchinja ngamia, na kurudia Hijja hiyo mwaka unaofuata.

b. **Baada ya Tahallul ya Kwanza:** Hijja yake haiharibiki, lakini anawajibika kuchinja mbuzi/kondoo.

## Uzushi na Makosa Yanayofanywa na Mahujaji

Kuna makosa na mambo ya uzushi (Bid'ah) ambayo yameenea miongoni mwa baadhi ya mahujaji kutokana na ujinga au kufuata mila potofu. Ni muhimu kuyajua ili kuyaepuka. Miongoni mwa hayo ni:

1. **Kuhusiana na Ihram:**
   a. Kuamini kwamba ni lazima kuhirimia kutoka msikiti fulani.
   b. Kuswali rakaa mbili za Ihram kama jambo la lazima.
   c. Kuacha kuoga au kubadilisha nguo za Ihram kwa kuamini kuwa uchafu ni sehemu ya ibada.
2. **Kuhusiana na Tawaf:**
   a. Kuanza Tawaf kabla ya Hajarul-Aswad (Jiwe jeusi) au baada.
   b. Kuhusisha kuomba dua maalum kwa kila mzunguko.
   c. Kugusa pembe zote za Al-Kaaba au kuta zake na kutabaruku.
   d. Kufanya Tawaf kwa niaba ya mtu mwingine aliye hai na mwenye uwezo.
   e. Kusongamana na kugusana na wanawake kwa makusudi.
   f. Kuzidisha maneno mengine zaidi ya yaliokuja katika dhikri hii

   رَبَّنَا آتِنَا فِي الدُّنْيَا حَسَنَةً وَفِي الْآخِرَةِ حَسَنَةً وَقِنَا عَذَابَ النَّار

   g. Kupita ndani ya Hijr Ismail (haichukuliwi kuwa ni sehemu ya Tawaf)
   h. Wanawake kudhihirisha mapambo (Kuvaa nguo zenye kuvutia, kujipamba, manukato n.k.)
   i. Kutamka nia ya Tawaf.
   j. Kukosa udhu katika Tawaf.

3. **Kuhusiana na Sa'yi:**
   a. Kuanza Sa'yi kutoka Marwa badala ya Swafa.
   b. Kuhesabu kwenda na kurudi kama mzunguko mmoja.

RIHLATUL HUDAA
HAJJ & UMRAH AGENCY

4. **Kuhusiana na Arafa:**
    a. Kupanda Jabal Ar-Rahmah (Mlima wa Rehema) na kuusalia au kuupangusa kwa kutaka baraka.
    b. Kuamini kwamba ni lazima kusimama karibu na mlima huo.
    c. Kusimama nje ya mpaka wa Arafa au kuondoka kabla ya jua kuzama.

5. **Kuhusiana na Muzdalifa:**
    a. Kuokota mawe kutoka Muzdalifa pekee na kuamini kuwa mawe ya sehemu nyingine hayafai.
    b. Kuyaosha mawe hayo kabla ya kuyatumia.

6. **Kuhusiana na Kurusha Jamarat:**
    a. Kurusha mawe kwa hasira na kwa matusi.
    b. Kurusha vitu vingine kama viatu au mwavuli na vyenginevyo zaidi ya mawe.
    c. Kuamini kuwa unamrushia shetani.

*Ni muhimu kwa kila anayehiji na kufanya Umra kutafuta elimu sahihi na kufuata mwongozo wa Mtume* (ﷺ) *ili ibada zao zikubaliwe.*

RIHLATUL HUDAA
HAJJ & UMRAH AGENCY

# SEHEMU YA NANE: ZIYARA YA MASJID AL-NABAWI



Kutembelea mji wa Madina na kuswali katika Msikiti wa Mtume (ﷺ) ni jambo lenye fadhila kubwa, ingawa si sehemu ya ibada ya Hijja wala Umra. Hata hivyo, kwa kuwa mahujaji wengi hupata fursa ya kwenda Madina, ni muhimu kuelewa adabu na hukumu za ziyara hiyo.

## Hukumu ya Kutembelea Masjid al-Nabawi:

Ni Sunnah iliyohimizwa kusafiri kwa nia ya kwenda kuswali katika Msikiti wa Mtume (ﷺ). Nia ya safari isielekezwe kwenye kaburi, bali kwenye msikiti. Mtume (ﷺ) amesema:

**لَا تُشَدُّ الرِّحَالُ إِلَّا إِلَى ثَلَاثَةِ مَسَاجِدَ: الْمَسْجِدِ الْحَرَامِ، وَمَسْجِدِ الرَّسُولِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ، وَمَسْجِدِ الْأَقْصَى**

"Safari (za ibada) hazifungwi isipokuwa kwenda kwenye misikiti mitatu: Msikiti Mtakatifu (wa Makka), Msikiti wa Mtume (ﷺ) (wa Madina), na Msikiti wa Al-Aqsa (wa Yerusalemu)." (Sahih Al-Bukhari: 1189)

**Fadhila za Msikiti wa Mtume (ﷺ):**

صَلَاةٌ فِي مَسْجِدِي هَذَا أَفْضَلُ مِنْ أَلْفِ صَلَاةٍ فِيمَا سِوَاهُ، إِلَّا الْمَسْجِدَ الْحَرَامَ

"Swala moja katika msikiti wangu huu ni bora kuliko Swala elfu moja katika misikiti mingine, isipokuwa Msikiti Mtakatifu (Makka)."

(Sahih Al-Bukhari: 1190)

# Adabu za Ziyara:

1. **Kuingia Msikitini:** Unapoingia, tanguliza mguu wa kulia na usome dua ya kuingia msikitini.

بِسْمِ اللَّهِ، اَللّٰهُمَّ افْتَحْ لِي أَبْوَابَ رَحْمَتِكَ.

(Bismillāh, Allāhumma iftaḥ lī abwāba raḥmatik)

"Kwa jina la Allah, Ee Mola wangu! Nifungulie milango ya rehema Zako."

(Imepokelewa katika Sunan Ibn Majah, 771).

Kisha, swali rakaa mbili za *Tahiyyatul-Masjid* (maamkizi ya msikiti); na itakua vziuri ikiwa atapata nafasi ya kusali Rauwdha na kuomba dua.

Mtume (ﷺ) amesema:


ما بَيْنَ بَيْتي ومِنْبَري رَوْضَةٌ مِن رِياضِ الجَنَّةِ

"Kilicho kati ya nyumba yangu na mimbari yangu ni Bustani miongoni mwa bustani za Pepo."

(Imepokewa na Al-Bukhari na Muslim)

Hivyo, wanawavyuoni wanataja kuwa ni sehemu inayopendekezwa kukithirisha dua sana, kusali sunna na kumuombea dua Mtume na maswahaba zake.

RIHLATUL HUDAA
HAJJ & UMRAH AGENCY



2. **Kutoa Salamu kwa Mtume (ﷺ):** Baada ya kuswali, nenda kwa adabu na utulivu kwenye kaburi la Mtume (ﷺ). Simama mbele yake na useme:

"السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا رَسُولَ اللَّهِ وَرَحْمَةُ اللَّهِ وَبَرَكَاتُهُ"

(Assalamu 'alayka ya Rasul-Allah wa rahmatullahi wa barakatuh)**.**

Kisha, sogea kidogo kulia na utoe salamu kwa Abu Bakr As-Siddiq (radhiyallahu 'anhu), na kisha kwa Umar ibn Al-Khattab (radhiyallahu 'anhu).

3. **Kuzuru Maeneo Mengine:** Ni Sunnah pia kuzuru maeneo mengine ya kihistoria Madina kama vile Msikiti wa Quba, makaburi ya Al-Baqi', na makaburi ya mashahidi wa Uhud.



# MSIKITI WA QUBA NA FADHILA ZAKE

Msikiti wa Quba ni msikiti wa mwanzo uliojengwa katika historia ya kiisilamu na ni msikiti ulioasisiwa kwa imani na uchamungu. Allah anasema:

لَّمَسْجِدٌ أُسِّسَ عَلَى التَّقْوَى مِنْ أَوَّلِ يَوْمٍ أَحَقُّ أَن تَقُومَ فِيهِ فِيهِ رِجَالٌ يُحِبُّونَ أَن يَتَطَهَّرُوا وَاللَّهُ يُحِبُّ الْمُطَّهِّرِينَ.

….. Msikiti ulio jengwa juu ya msingi wa uchamngu tangu siku ya mwanzo unastahiki zaidi wewe usimame ndani yake. Humo wamo watu wanao penda kujitakasa. Na Allah anawapenda wanao jitakasa (108).

**Fadhila za Msikiti wa Quba.**

Mtume ﷺ alikuwa akiutembelea msikiti wa Quba mara kwa mara, mara nyengine kwa kutembea kwa miguu na mara nyengine juu ya kipando na akaeleza kuwa atakae swali ndani ya msikiti huo atakua anaujira wa umrah.

عَنْ ابْنِ عُمَرَ قَالَ: كَانَ النَّبِيُّ ﷺ يَأْتِي مَسْجِدَ قُبَاءٍ كُلَّ سَبْتٍ مَاشِيًا وَرَاكِبًا.

“Kutoka wa Ibn ‘Umar, amesema: Mtume ﷺ alikuwa akifika msikitini Quba’ kila Jumamosi akitembea au akipanda mnyama.”

عَنِ سَهْلِ بْنِ حُنَيْفٍ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ ﷺ: «مَنْ تَطَهَّرَ فِي بَيْتِهِ ثُمَّ أَتَى مَسْجِدَ قُبَاءٍ فَصَلَّى فِيهِ صَلاَةً كَانَ لَهُ كَأَجْرِ عُمْرَةٍ»

“ kutoka kwa Sahl ibn Hunayf amesema: amesema Mtume wa Allah ﷺ: ‘Yeyote atakaejitoharisha (kuchukua udhu) nyumbani kwake, kisha akaja msikitini Quba’ na akaswali sala ndani yake, atakuwa na thawabu (malipo) kama ya ‘Umrah.’”

RIHLATUL HUDAA
HAJJ & UMRAH AGENCY



**Makosa ya Kuepuka Wakati wa Ziyara:**

1. Kusafiri kwenda Madina kwa nia ya kuzuru kaburi la Mtume (ﷺ) pekee. Nia sahihi iwe ni kuzuru Msikiti wa Mtume.
2. Kupangusa kuta za kaburi la Mtume (ﷺ) au chumba chake kwa ajili ya kutafuta baraka (Tabarruk).
3. Kuomba msaada kutoka kwa Mtume (ﷺ) badala ya kumuomba Allah.
4. Kuzuru makaburi mengine na kuyafanya kama mahali za ibada.
5. Kuwaomba maiti waliomo makaburini wakiwemo mashahidi wa vita vya badri na uhud.
6. Kuomba Msaada kwa Maiti: Kumuomba Mtume (ﷺ) au watu wengine waliozikwa hapo msaada, kwani dua na maombi yote huelekezwa kwa Allah pekee.
7. Kuswali Kuelekea Kaburi: Ni haramu kuswali kuelekea kaburi. Qibla cha Waislamu ni Al-Kaaba pekee.

RIHLATUL HUDAA
HAJJ & UMRAH AGENCY

# SEHEMU YA TISA: MAS-ALA MUHIMU

## Hijja kwa Niaba (الحج عن الغير):

Inajuzu kumfanyia mtu mwingine Hijja au Umra, ikiwa mtu huyo amefariki au ni mgonjwa asiye na matumaini ya kupona, na alikuwa na uwezo wa kuhiji. Sharti ni kwamba yule anayemhijia mwenzake awe ameshajihijia yeye mwenyewe kwanza. Dalili ni Hadith ya

mwanamke aliyemuuliza Mtume (ﷺ) kuhusu baba yake mzee ambaye hawezi kukaa kwenye kipando, akamruhusu amhijie (Sahih Al-Bukhari: 1855).

## Hijja ya Mtoto Mdogo:

Hijja ya mtoto mdogo ambaye hajabaleghe inasihi na anapata thawabu, na wazazi wake pia wanapata thawabu. Hata hivyo, Hijja hiyo haimuondolei wajibu wa Hijja ya Uislamu atakapokuwa mtu mzima na mwenye uwezo.

## Umra katika Ramadhani:

Kufanya Umra katika mwezi wa Ramadhani kuna fadhila kubwa sana. Mtume (ﷺ) amesema:

**فَإِنَّ عُمْرَةً فِي رَمَضَانَ تَقْضِي حَجَّةً مَعِي**

"Hakika Umra katika Ramadhani inalingana (kwa thawabu) na Hijja pamoja nami."

(Sahih Al-Bukhari: 1863)

# SEHEMU YA KUMI: MAELEZO YA KINA KUHUSU HADIY NA UDHIYA

**Hadiy (الهدي) na Udhiya (الأضحية)**

## Tofauti kati ya Hadiy na Udh-hiya:

*Hadiy* ni mnyama anayechinjwa huko Makka kwa ajili ya ibada ya Hijja au Umra, na ni wajibu kwa wanaofanya Hijja ya Tamattu' na Qiran. *Udhiya* ni mnyama anayechinjwa siku za Eid al-Adha popote pale, si lazima kuwa Makka.

RIHLATUL HUDAA
HAJJ & UMRAH AGENCY

**Wanaotakiwa Kuchinja Hadiy:**

1. Wanaofanya Hijja ya Tamattu' (التمتع).
2. Wanaofanya Hijja ya Qiran (القران).
3. Anayefanya Umra katika miezi ya Hijja na kisha anabaki Makka hadi Hijja.

Dalili yake ni kauli ya Allah:

فَمَن تَمَتَّعَ بِالْعُمْرَةِ إِلَى الْحَجِّ فَمَا اسْتَيْسَرَ مِنَ الْهَدْيِ ۚ فَمَن لَّمْ يَجِدْ فَصِيَامُ ثَلَاثَةِ أَيَّامٍ فِي الْحَجِّ وَسَبْعَةٍ إِذَا رَجَعْتُمْ ۗ تِلْكَ عَشَرَةٌ كَامِلَةٌ

"Basi mwenye kufanya Tamattu' (kufurahia) kwa Umra hadi Hijja, basi achinje mnyama alie mwepesi kumpata. Na asiyepata, basi afunge siku tatu katika Hijja, na saba mtakaporejea. Hizo ni kumi kamili."

(Surat Al-Baqarah: 196)

**Masharti ya Mnyama wa Hadiy:**

1. **Aina:** Awe ni ngamia, ng'ombe, mbuzi, au kondoo.
2. **Umri:** Ngamia awe na umri wa miaka mitano au zaidi, ng'ombe awe na miaka miwili, mbuzi na kondoo wawe na mwaka mmoja.
3. **Afya:** Awe mzima, bila kasoro kubwa kama upofu, ulemavu, au ugonjwa mbaya.

**Wakati wa Kuchinja:**

Wakati wa kuchinja Hadiy huanza siku ya Eid (10 Dhul-Hijjah) baada ya Swala ya Eid, na unaendelea hadi jua kuzama siku ya 13 ya Dhul-Hijjah (siku ya mwisho ya Tashriq).

**Jinsi ya Kugawa Nyama:**

Ni Sunnah kugawa nyama ya Hadiy katika sehemu tatu:

1. Sehemu moja kwa mchinjaji mwenyewe.
2. Sehemu moja kwa marafiki na jamaa.
3. Sehemu moja kwa masikini na wahitaji.

Hata hivyo, ikiwa ni Hadiy ya wajibu (kama ya Tamattu'), ni halali kula sehemu yake, tofauti na Fidya ambayo yote inagawiwa masikini.

RIHLATUL HUDAA
HAJJ & UMRAH AGENCY

# MASWALI YANAYOULIZWA MARA KWA MARA

**1. Je, ni lazima kufanya Umra kabla ya Hijja?** Hapana, si lazima. Umra ni ibada tofauti na Hijja. Mtu anaweza kufanya Hijja bila kufanya Umra, na anaweza kufanya Umra bila kufanya Hijja.

**2. Je, mwanamke anaweza kufanya Hijja au Umra bila mahram?** Hapana. Ni sharti kwa mwanamke kusafiri na mahram wake (mume au wanaume ambao ni haramu kwake kuwaoa kama baba, kaka, ndugu, mjomba, n.k.). lakini zipo kauli za wanavyuoni zinazojuzisha hilo kama tulivyotangulia kueleza katika kurasa nambari 4-5.

**3. Je, ninaweza kufanya Hijja kwa niaba ya mzazi wangu aliye hai?** Ikiwa mzazi wako ni mgonjwa asiye na matumaini ya kupona na hawezi kusafiri, unaweza kumfanyia Hijja. Lakini ikiwa ni mzima na mwenye uwezo, hawezi kumfanyia mtu mwingine Hijja.

**4. Je, naweza kubadilisha nia yangu baada ya kuingia Ihram?** Ndiyo, unaweza kubadilisha kutoka Ifrad au Qiran kwenda Tamattu', lakini si kinyume chake. Hii ni kwa mujibu wa mwongozo wa Mtume (ﷺ) kwa maswahaba zake.

**5. Je, ikiwa nimesahau kurusha Jamarat siku moja, nifanye nini?** Ikiwa umesahau kurusha siku moja, unaweza kurusha siku inayofuata. Lakini ikiwa umesahau kabisa hadi umekwisha ondoka Mina, unawajibika kuchinja mnyama (Fidya).

**6. Je, ninaweza kufanya Tawaf kwa gari la magurudumu ikiwa siwezi kutembea?** Ndiyo, ikiwa una udhuru wa kisheria kama ugonjwa au uzee, unaweza kufanya Tawaf kwa gari la magurudumu au kubebwa.

**7. Je, mwanamke aliye katika hedhi anaweza kufanya nini?** Mwanamke aliye katika hedhi au nifasi haruhusiwi kufanya Tawaf. Lakini anaweza kufanya matendo mengine yote ya Hijja kama Wuquf Arafa, kukaa Muzdalifa, kurusha Jamarat, n.k. Ikiwa hedhi yake itaisha, atajitakasa na kufanya Tawaf. Ikiwa haitaisha, Tawaf Al-Wada' haimuhusu.

RIHLATUL HUDAA
HAJJ & UMRAH AGENCY

**8. Je, ni lazima kurusha Jamarat kwa mikono yangu mwenyewe?** Ndiyo, ni lazima kurusha kwa mkono wako mwenyewe ikiwa unaweza. Lakini ikiwa una udhuru (ugonjwa, uja mzito, n.k.), unaweza kumwagiza mtu mwingine akurushe kwa niaba yako.

# SEHEMU YA KUMI NA MOJA: HITIMISHO

**Hitimisho**

Kwa kumalizia, tunamshukuru Allah (Subhanahu wa Ta'ala) kwa kutuwezesha kukamilisha kitabu hiki kidogo, ambacho tumelenga kiwe mwongozo rahisi na wenye manufaa kwa ndugu zetu Waislamu wanaozungumza Kiswahili. Ibada ya Hijja na Umra ni safari ya kiroho, safari ya kumuelekea Mola Muumba, na ni fursa adhimu ya kusamehewa dhambi.

Nasaha zetu kwa kila anayejaliwa kupata fursa hii tukufu ni kuhakikisha anajitayarisha kwa elimu sahihi kabla ya safari, ili aweze kutekeleza ibada yake kwa kufuata mwongozo wa Mtume Muhammad (ﷺ), kwani yeye ndiye aliyetuambia: "Chukueni kutoka kwangu ibada zenu za Hijja."

Jambo la msingi katika ibada zote ni Ikhlasi (kumtakasia nia Allah) na Mutaba'ah (kumfuata Mtume ﷺ). Basi, na iwe Hijja yetu na Umra yetu ni kwa ajili ya Allah pekee, na iwe inafuata Sunnah. Tuepuke ria (kujionyesha), mabishano yasiyo na faida, na mambo yote ya uzushi ambayo hayana msingi katika dini.

Tunamuomba Mwenyezi Allah azikubali Hijja na Umra zetu, atusamehe madhambi yetu, na atujaalie mwisho mwema. Aamiin.

**رَبَّنَا تَقَبَّلْ مِنَّا إِنَّكَ أَنتَ السَّمِيعُ الْعَلِيمُ.**

"Mola wetu, pokea kutoka kwetu, hakika Wewe ndiwe Mwenye kusikia, Mjuzi."

**سُبْحَانَ رَبِّكَ رَبِّ الْعِزَّةِ عَمَّا يَصِفُونَ، وَسَلَامٌ عَلَى الْمُرْسَلِينَ، وَالْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ**

"Ametakasika Mola wako, Mola wa utukufu, na wasifuzo. Na amani iwe juu ya Mitume. Na sifa njema zote ni za Mwenyezi Mungu, Mola wa walimwengu wote."

---

**تم بحمد الله وتوفيقه**

**Imekamilika kwa Neema na Msaada wa Mwenyezi Mungu**

**Mwandishi:** أبي أنعم لقمان ناصر آل باشو

**Tarehe ya Kukamilisha:** ١٤٤٧ هـ / ٢٠٢٥ م